



EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

MAOMBI YA TAARIFA YA KUONYESHA NIA KWA AJILI YA HUDUMA YA BIMA/UDALALI WA BIMA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMBUKUMBU NA. 0010006783

TOTAL East Africa Midstream B.V (Kampuni) , Kampuni ya Mafuta na Gesi, inaalika madalali wa Bima wenye uzoefu na sifa kuonyesha nia kwa ajili ya kutoa huduma za udalali wa bima katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP).

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha shughuli za uhandisi, ujenzi, uendeshaji na usimamizi wa bomba la kusafirisha Mafuta ghafi lililofukiwa chini ya ardhi na lililofunika ili kutunza joto linalokatisha nchi za Uganda na Tanzania na lenye mfumo wa umeme wa kulipasha joto, miundombinu ya juu ya ardhi na eneo la kuhifadhi Mafuta lililo pembezoni mwa Bahari katika eneo la Chongoleani, karibu na bandari ya Tanga nchini Tanzania. Mradi wa EACOP ni Mradi unaowezeshwa kifedha na inategemewa wakopeshaji wanaweza kuhitaji kufahamu juu ya mpango wa bima na udhamini bima.

MAELEZO MAFUPI YA HUDUMA:

Mradi wa EACOP unahitaji mpango Madhubuti wa bima na udhamini bima utakaotumika katika awali ya Mradi kama ifuatavyo na kuandaliwa na dalali wa bima anayehusika na:

- Kutengeneza sera ya kazi za awali kulingana na mahitaji,
- Kutengeneza udhamini wa bima katika soko la udhamini wa bima la Kimataifa na la hapa nchini kama inavyohitajika kisheria na katika mikataba mbalimbali,
- Kuandaa na kukamilisha uchaguzi wa watoa huduma za bima nchini Tanzania na Uganda,
- Kukidhi kikamilivu matakwa ya wawezeshaji wa Mradi kifedha,

- Kutekeleza sera katika kipindi cha hatua zote za Mradi,
- Kuhusisha na mpango wa bima wa Tilenga.

Tilenga ni Mradi uliopo katika wilaya za Buliisa na Nwoya katika ziwa Albert, inajumuisha utengenezaji wa maeneo 6 ya Mafuta na uchimbaji wa visima takriban 400 katika maeneo 31.

VIGEZO MUHIMU:

Makampuni yanayoonyesha nia yanaalikwa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili wa kampuni au shirika kwa ajili ya kutoa huduma tajwa.
- Uzoefu wa kuandaa mipango ya bima katika miradi ya Mafuta na gezi kwa ngazi za Kimataifa na kitaifa.
- Uzoefu wa kufanya kazi na wawezeshaji wa kifedha wa Kimataifa katika miradi inayowezeshwa kifedha.
- Uwezo wa kusimamia sera baada ya kuzianziba, bila kujikita tu kwenye utoaji wa sera, udhamini wa bima za juu pamoja na madai, kujibu maswali ya wanufaika wa bima katika hatua zote za Mradi, kutoa usaidizi wa kiutaalamu, kusimamia, kufuatilia uhalisia wa udhamini wa bima.
- Uthibitisho wa kuwa na rasilimali zinazohitajika – wahuusika wenye vigezo na timu itakayofanya kazi na EACOP katika vipengele vyote viinavyohusiana na mpango.
- Uwezo wa kifedha wa kutekeleza huduma zinazohitajika.

Makampuni yenye nia, ambayo yana uwezo na rasilimali za kutoa huduma zilizotajwa hapo juu yanatakiwa kutuma taarifa ya kuonyesha nia iliyoandaliwa kwa lugha ya kiingereza pamoja na nyaraka tajwa kupitia barua pepe: **EACOP.EOI-BROKERS@total.com** (ukubwa usiozidi MB20) hadi kufikia saa **11:00** jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe **2 Juni 2021**.

Muhimu: Kwa ajili ya kutengeneza orodha ya makampuni ya Awali yenye vigezo, Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na makampuni yenye nia. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya Awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA).